KILIMANJARO MARATHON 2022, TIGO KILOMETA 21 (TIGO HALF MARATHON), KILOMETA 5 (GRAND MALT FUN RUN)

VIGEZO & MASHARTI YA KUZINGATIA WAKATI WA KUJISAJILI KILIMANJARO PREMIUM LAGER MARATHON (KILOMETA 42), TIGO KILOMETA 21 (TIGO HALF MARATHON) AU GRANDMALT KILOMETA 5 (GRAND MALT FUN RUN) – HIVI NDIO VIGEZO NA MASHARTI YA KURIDHIA KABLA YA KUJISAJILI:

Usajili huu unaendana na maelezo yaliyotolewa katika tovuti na kama ilivyoainishwa hapa chini, kuhusu Kilimanjaro Marathon 2022 (tukio lenyewe). Nathibitisha kuwa nimesoma na nimeelewa vigezo na masharti ya mkataba huu kama ilivyoambatanishwa. Natangaza wazi kuwa ninavyo vigezo na nastahili kushindana kama ilivyoainishwa kwa kuzingatia kanuni zilizowekwa na Shirikisho la Kimataifa la Riadha (IAAF) na Chama Cha Riadha Tanzania (RT). Kwa kusaini makubaliano haya nathibitisha kuwa sitaidai Kilimanjaro Marathon wala wafanyakazi wake endapo nitapoteza chochote au kuumia wakati wa tukio hili. Pia nathibitisha kuwa najiweza na nina uwezo wa kusaini binafsi au kuombwa kusaini kwa niaba ya mtu mwingine na nakubaliana na vigezo na masharti yaliyowekwa katika fomu hii ya usajili.

1. Ninaridhia maelezo na pia ninakubali kwamba mashindano haya yaliyoandaliwa na kusimamiwa na mratibu wa tukio hili, linaweza kuwa na athari mbalimbali kama vile kuumia, kuugua ghafla, kifo au uharibifu wa vifaa vya michezo na mali aina nyingine ya washiriki.

2. Ninakubali kuwa athari zitakazotokea wakati wa tukio hili, ni pamoja na, lakini hayana ukomo na athari zitakazotokana na juhudi zangu na uwezo wangu kama mwanariadha anayekimbia au anayetembea au mshiriki mwingine yeyote kwa jina lake, lishe yangu na unywaji wa maji, afya yangu kabla, wakati na baada ya tukio hilo, maeneo ambayo washiriki watapitia wakati wa mashindano hayo, barabara, hali ya hewa, hali ya maji, msongamano wa magari, vitendo vitakavyotendwa na washiriki wengine, mratibu wa tukio, wafadhili wa mashindano haya na viongozi wake, wawakilishi, mawakala na wale waliopewa majukumu wakati wa mashindano hayo. Ninaridhia na kukubali kujiondoa kushiriki kwenye mashindano haya iwapo nitashauriwa au kuamriwa na mratibu wa tukio hili kufanya hivyo au ikiwa, wakati wowote, nitahisi au nitazingatia athari yoyote

isiyo ya kawaida au hali isiyo salama na nina wasiwasi kwa njia yoyote kuwa sio salama kwangu kuendelea kushiriki mashindano haya au ikiwa mimi, kwa njia yoyote ninahisi kutoweza au sitakuwa salama au sistahili kuendelea na mashindano haya.

3. Ninathamini na kuelewa athari zilizo katika mashindano haya na ushiriki wangu katika tukio hili. Ninakubali kuweko na athari za namna hii na ninathibitisha ya kuwa ninashiriki katika mashindano haya kwa hiari yangu mwenyewe na kuhusika moja kwa moja na athari zitakazonipata kwa njia moja au nyingine.

4. Ninaahidi kufuata na kutii sheria zote za mashindano haya pamoja na maagizo yote yaliyotolewa na mratibu wa mashindano haya, wakuu wa mashindano haya, wawakilishi wake, mawakala wake na nadhibitisha mbele ya wote hawa ya kuwa ninaelewa ya kuwa mashindano haya yameidhinishwa na shirikisho la kimataifa la vyama vya riadha (IAAF), chama cha mashindano ya kimataifa yam bio ndefu (AIMS) na chama cha riadha Tanzania (RT).

5. Ninaelewa na kuridhia ya kuwa kuna uwezekano wa mimi kupigwa picha kabla, wakati au baada ya Tukio. Ninakubali na kuridhia ya kuwa mratibu wa mashindano, wadhamini na viongozi walioandaa mashindano haya, wawakilishi wao, mawakala wao na wafadhili wao wanaweza kutumia picha nitakazopigwa pamoja na majina yangu kwa ajili ya tukio lolote linalohusiana na mashindano haya ambayo mimi nitakuwa mshiriki wake na katika hafla nyingine yoyote itakayoandaliwa na mratibu wa mashindano haya wakati wowote baada ya mashindano haya.

6. Ninatambua ya kuwa, kwa sababu ya ushiriki wangu katika hafla hiyo, waandaaji wa hafla hiyo watawasiliana nami mara kwa mara (kwa njia ya barua za kielektroniki, huduma ya ujumbe mfupi na/au simu) kwa madhumuni ya: (i) mawasiliano kuhusiana na tukio au habari zinazohusiana zinazohuasiana na tukio hilo; (ii) kutangaza bidhaa na/au huduma ambazo zinaweza kunisaidia katika kuandaa na kufanya kazi katika tukio hilo; na/au (iii) kutangaza riadha na/au hafla zingine zinazoendeshwa na/au kusimamiwa na mratibu wa tukio hili. Kwa hivyo, ninakubaliana na kuridhia mawasiliano yoyote ya aina hii.

7. Wazazi au walezi wanaoruhusu ushiriki wa watoto katika mashindano haya, watathibitisha hayo kwa kutia saini fomu maalum ya kuridhia ushiriki wa watoto wao kama ishara ya kukubali ushiriki wa watoto hao pia kukubaliana na maelezo yote yaliyotajwa hapo juu hii ikiwa ni pamoja na kutokuhusika au kudai ya fidia aina yoyote kwa niaba ya watoto watakaoshiriki kama kutakuwa na athari zitakazowapata. Vivyo hivyo endapo mshiriki atateua mtu mzima kushiriki, pia makubaliano yatakuwa kama ilivyoanishwa hapo juu.

8. Kwa hivyo najitoa kadiri inavyowezekana kisheria, dhidi ya madai yoyote yatakayotokana na ushiriki wangu katika mashindano haya, bila kujali ni ya kiwango gani, athari hizo bila ya ukomo wa aina yoyote ni pamoja na hasara ya aina yoyote, majeraha, madhara ya aina yoyote, ugonjwa wa ghafla wakati wa tukio, kifo au uharibifu wa aina yoyote utakaokuwa umesababishwa na sababu yoyote ile moja kwa moja kwa kitendo chochote au kutokuwepo, pamoja na vitendo vya uzembe vya upungufu wa pande zote, pamoja na madai yoyote yanayohusiana na hasara yoyote, wa uharibifu, upotevu wa faida au madai yoyote na madai yoyote ya wategemezi wangu wanaotokana watakaoshiriki tukio hili au hafla zinazohusiana na tukio hili wala sitahusika na madai yanayotokana na ushiriki wangu katika mashindano haya.

9. Ninathibitisha kwamba ninaelewa umuhimu na maana ya maelezo ya kuondolewa kipengele cha madai na fidia na kwamba kwa kukubali hili, ninaondoa haki ya kisheria ya kudai fidia (kwa niaba yangu mwenyewe na kwa niaba ya wategemezi wangu). Ninakubali kwamba nimekuwa huru katika kupata ushauri wa kisheria na/au ushauri mwingine wa ziada juu ya hali na athari za vifungu vyote vya hakiki ya dhima, msamaha na fidia na kwamba nimekubaliana na ushauri huo wa kisheria na/au ushauri mwingine niliopewa na kwamba nimechukua uamuzi huu bila kulazimishwa.

10. Ninathibitisha kwamba ninaelewa na kuridhia ya kuwa hakuna marejesho au mbadala wa aina yoyote iwapo kutakuwa na mabadiliko yoyote katika mashindano ya Mbio za Kilimanjaro Premium Lager Marathon, Tigo Half Marathon (21km) au mbio za Km 5 (Fun Run) baada ya viingilo kulipwa na kuthibitisha ushiriki.

11. Zaidi ya yote haya washiriki wanaridhia na kukubali ya kwamba tukio hili linaweza kufutwa au kuahirishwa, kutokana na sababu zilizo nje ya uwezo wa wandaaji wa mashindano, sababu ni (Matukio yanayotokana na mapenzi ya Mungu, migomo, vita, ghasia, moto, mafuriko, machafuko, sababu za kisheria, uasi, ugonjwa, amri ya Serikali na/au mizozo ya kibiashara) na kwamba katika hali kama hizo, mratibu wa tukio hatatakiwa kurudisha ada za viingilio vya mashindano hayo.

12. Washiriki wanakubali kwamba watatumia vifaa vya kujikinga (PPE) kama ilivyoagizwa na waandaaji wa mashindano hayo kulingana na hatua za sasa za kimataifa zinazolenga kuzuia maamukizi ya ugonjwa wa Uviko 19 (Covid-19), pamoja na kufuata masharti ya umbali wa watu kukaa kama inavyoelekezwa na wataalam wa afya katika maeneo yaliyopangwa kuanzia na kumalizia mashindano haya.